

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI NA TANO

22 MEI, 2026



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI NA TANO – TAREHE 22 MEI, 2026

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

410. MHESHIMIWA AMINA ALI MZEE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali inachukua hatua zipi kupunguza tatizo la ajira kwa Vijana wanaomaliza masomo.

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

411. MHESHIMIWA MABULA JOHNSON MAGANGILA (MSALALA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, upi mpango wa Serikali wa kuongeza Shule za Sekondari katika Halmashauri ya Msalala.

412. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESHER KABATI (KILOLO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Barabara ya kutoka Ilula – Image – Ibumu itajengwa kwa kiwango cha lami.

**413. MHESHIMIWA KUNTI YUSUPH MAJALA
(CHEMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, nini mkakati wa Serikali wa kutatua changamoto ya uhaba wa Madawati katika Wilaya ya Chemba kwa Shule za Msingi na Sekondari.

**414. MHESHIMIWA DKT. OSCAR ISHENGOMA KIKOYO
(MULEBA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Stendi ya kisasa katika Wilaya ya Muleba.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**415. MHESHIMIWA EDIFONSI JOACKIM KANONI
(KALAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Chuo cha VETA Wilayani Kalambo.

WIZARA YA UJENZI:

416. MHESHIMIWA ERIC JAMES SHIGONGO (BUCHOSA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kivuko cha MV. Kome kutoka Nyakarilo hadi Kome.

417. MHESHIMIWA ZUENA ATHUMANI BUSHIRI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa Barabara ya Holili – Tarakea.

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

418. MHESHIMIWA MARYAM AZAN MWINYI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali imeweka mikakati gani ya kulinda Watoto walio katika mazingira hatarishi ikiwemo Watoto yatima na wenye Ulemavu.

WIZARA YA KILIMO:

419. MHESHIMIWA ALLY YAHYA MHATA (NANYUMBU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji katika Kata ya Likokona na Nangomba utaanza ikizingatiwa kuwa Mkataba ulishasainiwa.

WIZARA YA NISHATI:

420. MHESHIMIWA SARA MSAFIRI ALLY (MVOMERO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itatatua changamoto ya kuanguka kwa nguzo za Umeme katika Tarafa ya Mgeta.

421. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itapeleka umeme katika Vitongoji 169 vya Kata ya Ketare, Mihingo, Nyamang'uta, Mugeta, Salama, Hunyari, Mnyago na Nyamuswa.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**DODOMA
22 MEI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE**

